JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

OKTOBA 21, 2020

ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 4.2 IKIWEMO KODI YA SERIKALI KUTOKA KAMPUNI YA UWINDAJI YA OBC ZAOKOLEWA NA TAKUKURU ARUSHA KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA 2020

Ndugu Waandishi wa Habari,

Leo tumewaita hapa kama ulivyo utaratibu wa ofisi wa kutoa taarifa kwa wananchi juu ya kazi ya mapambano dhidi ya rushwa inayofanywa na ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha kwa kila kipindi cha robo mwaka.

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Septemba 2020, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007. Utekelezaji wa majukumu hayo ya TAKUKURU kwa mujibu wa sheria umeenda sanjari na kuzingatia maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali kwa lengo la kuhakikisha kwamba vitendo vya rushwa vinadhibitiwa, mali za umma zinalindwa na haki za wananchi zinazingatiwa.

Ndugu Waandishi wa Habari;

Katika kipindi tajwa, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha katika jukumu la kulinda Mali za Umma na kutetea haki za wananchi katika makundi yao mbalimbali, imefanikiwa kuokoa fedha taslimu jumla ya shilingi Bilioni nne Milioni Mia Mbili na Themanini, Laki Nne na Elfu

Arobaini na Kumi na Moja (**Sh. 4,280,440,011/=**). Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

1. **KODI / MIKOPO YA SERIKALI:** Fedha kiasi cha shilingi bilioni tatu na milioni mia tano (**Sh. 3,500,000,000/-)** zimelipwa na Kampuni ya uwindaji wa kitalii ya Otterlo Business Corporation (OBC), Fedha kiasi cha shilingi Million Sitini (**Sh. 60,000,000/-)** zimelipwa na Kampuni ya ANICROP Services na hivyo kufanya jumla ya shilingi Bilioni tatu, milioni mia Tano Sitini (**Sh. 3,560,000,000/-)** ambazo ni kodi za serikali zilizokuwa zimekwepwa kulipwa na makampuni husika kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2018 na 2020. Aidha kiasi cha jumla ya shilingi Milioni Ishirini na Nane, Laki Tisa Sitini na Moja Elfu (**Sh. 28,961,000/-**) ni kodi na mikopo ya serikali iliyokuwa imekwepwa kurejeshwa na kufanyiwa ubadhirifu na wananchi na watendaji mbalimbali wa serikali katika nyakati tofauti tofauti, fedha hizi zote zimerejeshwa Serikalini.

2. **VYAMA VYA USHIRIKA:** Fedha jumla ya shilingi Milioni Tisini na Nane na Laki Tisa (**Sh. 98,900,000/-)** za Chama Kikuu cha Ushirika cha Arusha Cooperative Union (**ACU**) zilizokuwa zimefanyiwa ubadhirifu baada ya mali za chama hicho kuuzwa kwa watu wasio waaminifu, fedha kiasi cha Shilingi Milioni Nne Laki Tatu na Elfu Hamsini (**Sh. 4,350,000/-)** zililipwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) na fedha jumla ya shilingi Milioni Nane (**Sh. 8,000,000/=**) ni michango ya wanachama wa Mabaraza ya Wafugaji iliyokuwa imefanyiwa ubadhirifu na viongozi wa Mabaraza hayo.

3. **VICOBA NA SACCOS:** Shilingi Milioni Themanini na sita, Laki Tano Themanini na Tisa na Mia Moja (**Sh. 86,589,100/-)** ni mikopo ya Vicoba na Succos mbalimbali iliyokuwa haijarejeshwa kwa muda mrefu kinyume na taratibu.

4. **WATU BINAFSI NA MIKOPO UMIZA**: Jumla ya fedha kiasi cha shilingi Milioni Mia moja Tisini na nne, Elfu Sabini na Mbili, mia moja tisini (**Sh. 194,072,190/=**) ni madai ya watu binafsi mbalimbali na mikopo iliyokuwa imetolewa kwa riba kubwa na Taasisi za kifedha IVOJ Micro Credit Co. Ltd ya Jijini Arusha na Rhobi Credit Co. Ltd ya Karatu.

5. **MADAI YA WAJASIRIAMALI NA WAKULIMA:** Fedha kiasi cha shilingi Milioni Mia Mbili Themanini na Tisa, Laki Mbili Sitini na Moja elfu na Mia Tatu (**Sh. 289,261,300/-)** ni fedha zilizolipwa na Kampuni ya Kijenge Animal Products kwa Wakulima waliokuwa wamekiuzia kiwanda hicho bidhaa za kilimo lakini hawakuwalipa kwa muda mrefu na jumla ya fedha shilingi Milioni Tano Laki Tisa Hamsini na Sita, Mia nne Ishirini na Moja (**Sh. 5,956,421/=**) ni fedha za wakulima waliouza mazao yao kwa Kampuni ya TBL na Kampuni moja ya mbegu iliyopo Wilayani Monduli bila kupewa malipo yao.

Ndugu Waandishi wa Habari;

Hivyo kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2020, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Arusha imeokoa fedha kama ifuatavyo;

i.	Kodi ya Serikali	-	Sh. 3,593,311,000/=
ii.	Fedha za vyama vya ushirika	-	Sh. 111,250,000/=
iii.	Fedha za VIKOBA na SACCOS	-	Sh. 86,589,100/=
iv.	Fedha za watu binafsi na Mikopo umiza	-	Sh. 194,072,190/=
v.	Fedha za Wakulima na Wajasiriamali	-	Sh. 295,217,721/=
	Jumla ya fedha iliyookolewa ni	-	**Sh. 4,280,440,011/=**

Ndugu Waandishi wa Habari;

Mbali na kufanikisha uokoaji wa kodi za Serikali, ulipwaji wa madeni ya Vyama vya Ushirika na ya watu binafsi, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Arusha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa kutumia njia kuu tatu ambazo ni; Uchunguzi na Mashtaka, Uelimishaji Umma na Utafiti na Udhibiti huku ikiwashirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba madhara ya rushwa yanaeleweka vyema kwa jamii na hivyo kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa kila mmoja wao kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2020 TAKUKURU Mkoa wa Arusha, imeendelea kutekeleza

majukumu yake kupitia **Madawati ya Uchunguzi na Mashtaka, Uelimishaji Umma na Uzuiaji Rushwa** kama yafuatayo:-

1. UCHUNGUZI NA MASHITAKA:

A. TAARIFA ZILIZOPOKELEWA

Kwa kipindi tajwa jumla ya taarifa **415** zilipokelewa kutoka sekta mbalimbali. Taarifa hizi zilipelekea kufunguliwa kwa majalada **221** ya uchunguzi na majalada hayo yanaendelea kuchunguzwa na chunguzi zake zipo katika hatua mbalimbali. Taarifa **77** zilizoonekana kutokuwa na tuhuma za kuchunguzwa zilifungwa na taarifa **06** zilihamishiwa idara nyingine. Pia ushauri yakinifu ulitolewa kwa watoa taarifa kwa malalamiko **111** yaliyoonekana kutoangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

B: KESI MAHAKAMANI

Kwa kipindi tajwa, TAKUKURU (M) Arusha imefungua Mashitaka mapya Kumi na Moja (**11**) Mahakamani. Pia Mashitaka Hamsini na Saba (**57**) yaliendelea Mahakamani yakiwa katika hatua mbalimbali za kimahakama.

Aidha kwa kipindi hicho mashauri nane (**08)** yalitolewa uamuzi ambapo kati ya hayo, Jamhuri ilishinda mashauri saba (**07**).

2. ELIMU KWA UMMA:

TAKUKURU (M) Arusha imeendelea kufanya jitihada za kuelimisha Umma juu ya uelewa mpana wa dhana ya Rushwa na pia kuwakumbusha wajibu wao katika mapambano dhidi ya Rushwa. Katika kipindi tajwa TAKUKURU ilijikita zaidi katika kuuelimisha umma juu ya **Rushwa katika Uchaguzi**, kwa lengo la kuwawezesha wadau kuielewa vyema na kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU ili kuweza kudhibiti vitendo vya rushwa kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu. Uelimishaji huo ulifanyika kwa njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

Na	KAZI ILIYOFANYIKA	IDADI
1	SEMINA	50
2	MIKUTANO/MIJADALA	29
4	KUFUNGUA KLABU	01
5	KUIMARISHA KLABU	74
6	UANDISHI WA MAKALA	13
7	MAONESHO	03
8	TAARIFA KWA UMMA	08

3. UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi cha mwezi Julai – Septemba, 2020 TAKUKURU mkoani Arusha imefanya uchambuzi wa mifumo ya uendeshaji wa vyama vya ushirika (AMCOS) ili kubaini mianya ya rushwa iliyopo na hatimaye kupendekeza njia sahihi za kuziba mianya hiyo.

MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU Mkoa wa Arusha imetembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za Serikali ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Katika kipindi tajwa jumla ya miradi ya maendeleo kumi na mbili (12) imetembelewa na kukaguliwa.

Aidha katika kipindi tajwa, TAKUKURU mkoa wa Arusha ilifanya chambuzi nane (08) za mifumo na kuendesha warsha nane (08) juu ya ushuru wa huduma (service levy) katika Halmashauri na taratibu za ajira katika Kampuni za ulinzi.

4. MIKAKATI YA TAKUKURU (M) ARUSHA KWA KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA, 2020

Ndugu Waandishi wa habari;

TAKUKURU (M) wa Arusha imejiwekea mikakati madhubuti katika kuendelea na mapambano dhidi ya rushwa, hasa kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika tarehe 28, Oktoba 2020.

Lengo la kuweka mikakati hii ni kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu ya Kuelimisha, Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa ufasaha ili kuweza kufikia lengo la kuwa na Utawala Bora Nchini na kuitokomeza Rushwa.

Mikakati yetu inayotekelezwa ni kama ifuatayo;

i. KUTOA ELIMU YA RUSHWA

TAKUKURU (M) Arusha katika kipindi hiki kifupi kilichobaki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu, inaendelea kuelimisha jamii juu ya rushwa na madhara katika chaguzi za kisiasa kwa njia mbalimbali zikiwemo kuendesha semina, kufanya mikutano ya hadhara na kurusha vipindi vya Radio. Aidha TAKUKURU mkoa wa Arusha itaendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki vyema katika mapambano dhidi ya Rushwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ili kuweza kupata viongozi bora watakaotumia muda wao na rasilimali za nchi kwa manufaa ya wote.

ii. UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU (M) Arusha itaendelea kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ndani ya mkoa ili kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinazotolewa na serikali na wafadhili zinatumika kwa usahihi na miradi iliyokusudiwa inakamilika kwa wakati ili kuweza kuwanufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa.

KUFANYA UCHUNGUZI WA TAARIFA ZA VITENDO VYA RUSHWA

TAKUKURU (M) Arusha itaendelea kupokea na kufanyia uchunguzi taarifa zote za vitendo vya rushwa zitakazopokelewa ofisini sanjari na kuhakikisha kwamba wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua stahiki.

5. MWISHO

Ndugu Waandishi wa habari;

TAKUKURU (M) wa Arusha tunatoa shukrani zetu za dhati kwenu Waandishi wa Habari kwa kuendelea kuuhabarisha umma juu ya shughuli za mapambano dhidi ya rushwa zinazofanywa na Serikali kupitia TAKUKURU na tunazidi kuomba ushirikiano wenu.

Tunatumia nafasi hii kuwasihi wananchi wa mkoa wa Arusha kutofumbia macho vitendo vya rushwa na kuwa tayari kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Aidha tunawaasa wananchi kutumia nafasi yao ya kupiga kura kuchagua viongozi waadilifu na wenye nia ya dhati ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Pia TAKUKURU (M) Arusha inatoa rai kwa vyama vya siasa na wagombea wa nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu ujao kuhakikisha kwamba hawatumii rushwa kuwashawishi wapiga kura ili wawachague na badala yake wawaachie wananchi uhuru wa kuchagua wagombea wanaoona wanafaa kushika nafasi husika kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla. Aidha tunawaasa wagombea wote kufuata sheria, kanuni na taratibu na kujiepusha na vitendo vya rushwa kwani watakapobainika TAKUKURU haitasita kuchukua hatua kali dhidi yao.

KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU.

Imetolewa na:

James G. Ruge – 0738 150 063

KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA